# Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Siku 16 za Kampeini ya Uanaharakati: **Dondoo za kuzungumza kwenye vyombo vya habari**

## Historia

Ukatili Dhidi ya Wanawake hutokea duniani kote; mara nyingi huwa ni siri, mara kwa mara hupuuzwa na hukubalika kama jambo la kawaida. Katika kila wanawake watatu mmoja hufanyiwa Ukatili wa kimwili na / au Ukatili wa Kingono kutoka kwa mwenzi wake au mtu mwingine zaidi ya mwenzi wake katika maisha yake (WHO). Vyombo vya habari vina jukumu maalumu katika kuongeza maarifa, kubadili mitazamo na tabia katika jamii yetu. Sisi sote kwa makusudi katika mahusiano yetu kwa ushirikiano na vyombo vya habari wakati wa siku 16 za kampeni tunaweza kutumia nguvu hii yenye ushawishi mkubwa na kuanzisha fikra makini na mjadala wa kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na wasichana.

Mbali na kuongeza uelewa wa umma, vyombo vya habari vina jukumu muhimu katika kuwawajibisha viongozi na watunga sera kwa kutoa taarifa kwa umma kwa ujumla kuhusu sheria na hatua za serikali au ushinikizwaji wa masuala ya Ukatili Dhidi ya Wanawake. Wakati wa siku 16 za kampeni kipindi hiki tunaweza kuhamasisha na kutoa changamoto kwa viongozi wetu kutumia sauti zao na kuchukua hatua sasa, ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake katika jamii yetu.

## Ni pointi gani za mazungumzo kwenye vyombo vya habari?

Pointi za mazungumzo kwenye vyombo vya habari ni njia nzuri ya kuelezea mawazo makuu ya kampeni kwa uwazi, kwa ufupi na kwa sauti moja. Tumia pointi za mazungumzo hapo chini kukuongoza (na wenzako wengine) ushirikiano na vyombo vya habari, wakati wa siku 16 za kampeni. Kwa mfano, kama umekaribishwa kwenye redio / kipindi cha majadiliano katika luninga, yanayoongozwa na mwandishi wa habari au kuandika makala gazetini kwa kutumia pointi katika kuzungumza na kuweka kesi wazi na kueleweka. Kushirikisha, kufanya mapitio na kuchagua pointi zinazolingana na mazingira yako ili kudumisha kauli mbiu yenye nguvu!

## Jinsi ya kutumia pointi za mazungumzo kwenye vyombo vya habari

### 1. Rekebisha ilingane na mazingira yako

a. Ndani ya kifurushi cha kuchukua hatua na utetezi kuna “karatasi kazi”. Karatasi hii lazima itumike kukusaidia kuweka mazingira ya kampeni za kikanda kwa mahitaji ya ngazi maalumu ya kitaifa au ngazi ya jamii ambayo ni muhimu kwa mazingira yako - inaweza kukusaidia kuamua kwa ufanisi zaidi na kuweka mikakati ya ushiriki wa viongozi katika kuchukua hatua.

b. Kabla ya kutumia pointi za mazungumzo haya, tafadhali kamilisha karatasi kazi katika kifurushi cha kuchukua hatua na utetezi, hii itahakikisha kwamba mahitaji maalumu unayowapa viongozi wenu, katika sehemu ya mwisho ya pointi za mazungumzo hayo, itakuwa muhimu kulingana na mazingira yako.

c. Fanya marekebisho ya takwimu zinazohitajika kwa utafiti ikiwa ni pamoja na taarifa maalumu kwa nchi yako / kanda / jimbo / wilaya.

**2. Rejea karatasi kazi na pointi za mazungumzo kwenye vyombo vya habari. Kisha fanya nyongeza katika sehemu A, B, na C kama ilivyoelekezwa hapo chini:**

a. Fanya nyongeza ya kifungu B na takwimu za kitaifa / ngazi za msingi kwenye gharama za kiuchumi za ukatili katika nchi yako ikiwa nchi yako imefanya utafiti.

b. Fanya marekebisho ya kifungu C kutumia muandiko wa italiki

## Mapendekezo ya pointi za mazungumzo

Tunakuhimiza kutumia mazungumzo haya kuhamasisha na kutoa changamoto kwa viongozi wenu kutumia sauti zao na kuchukua hatua za kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake kwa kuongea kwa uwazi kuhusu ukatili na kutoa rasilimali zinazohitajika ili kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.

### Sehemu A

- Ukatili Dhidi ya Wanawake ni "kitendo chochote cha kutumia nguvu kimwili au kwa maneno, kutishiwa na kuhatarisha maisha, yanayomlenga moja kwa moja kwa mwanamke binafsi au msichana na kusababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia, udhalilishwaji au kunyimwa uhuru na hivyo yanachangia kumweka mwanamke katika hadhi ya chini"
- Kuna aina 4 za ukatili dhidi ya wanawake:
  - kimwili
  - kingono
  - Kihisia
  - kiuchumi
- Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana ni ishara kubwa ya kutokuwa na usawa wa kijinsia na ukiukwaji wa haki za kijamii
  - Unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana hutokea duniani kote, mmoja (1) katika wanawake watatu (3) hufanyiwa ukatili wa kimwili / au wa kingono kutoka kwa mwenzi wake (WHO).
  - Katika kanda tunaendelea kuwa na viwango vya juu mno visivyo kubalika vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana; asilimia 36.6 ya wanawake hufanyiwa ukatili (WHO 2013).

    Ingiza takwimu muhimu katika ngazi ya kitaifa au kijamii, unaweza kupata takwimu hizi kutoka utafiti wa Idadi ya watu na Afya, WHO Tathmini ya dunia nk
  - Wanawake na wasichana hufanyiwa Ukatili ni matokeo ya kutokuwepo na usawa wa kijinsia na unyanyasaji.

- Wasichana na wanawake mara nyingi huishi kwa hofu katika mazingira mbalimbali- majumbani, shuleni, katika jamii zao, sehemu zenye migogoro na hata nyakati za amani.
- Ukatili Dhidi ya Wanawake ni mfumo wa kijamii ambao huundwa na mfumo dume ambao huwapa wanaume mamlaka zaidi kuliko wanawake. Kanuni hizi huruhusu wanaume kudhibiti vitendo na miili ya wanawake wakati mwingine kusababisha ukatili.
- Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana unaonekana kuwa ni kitendo cha kawaida katika jamii zetu. Hii haiweki mbali ukweli kwamba haukubaliki na ni ukiukwaji wa haki.

## Sehemu B

- Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana una madhara makubwa yanayoweza kudumu vizazi hadi vizazi. Ni ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na kikwazo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
  - Wanawake na wasichana inapelekea kuwa na uwezo mdogo wa kutumia ujuzi wao katika jamii, inapelekea kutengwa na kubaguliwa na jamii;
  - Wanawake na wasichana hupunguza au kupoteza elimu, ajira, au fursa ya ushiriki kijamii na kisiasa;
  - Watoto wanaoshuhudia ukatili wanauwezekano wa kuwa na matatizo kihisia na kitabia; hufanya vibaya shuleni na wako katika hatari ya kuchochea au kukabiliwa na ukatili katika siku zijazo.
  - Kuna matumizi makubwa (katika ngazi ya mtu binafsi, familia na bajeti katika sekta ya umma) katika matibabu, ulinzi, mahakama na huduma za jamii
  - Kutokana na ukatili wanawake hupoteza siku za kufanya kazi, hupunguza uzalishaji na kipato hupungua
- Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana huongeza mazingira hatarishi kwa mwanamke na matatizo ya kiafya ya muda mfupi na mrefu na huweza kusababisha kupoteza maisha; Ukatili Dhidi ya Wanawake ni tishio kubwa kwa afya ya wanawake. Tafadhali ingiza kama zipo takwimu zozote juu ya gharama za Ukatili Dhidi ya Wanawake katika nchi yako/ kikanda / jimbo / wilaya

## Sehemu C

Ukatili Dhidi ya Wanawake ni suala linalohitajika kushughulikiwa kwa haraka sasa; kila mtu ana sehemu ya kufanya katika kukomesha Ukatili. Viongozi wetu wana jukumu muhimu la kufanya ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa viongozi wetu (wa kisiasa, wataalam na viongozi washauri) katika ngazi zote kwa:

- Kuonyesha uongozi kwa kuvunja ukimya na kujiunga na ongezeko kubwa la vilio; kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana na kutetea usawa wa kijinsia
- Kutengeneza mpango mkakati wa kitaifa wa pamoja na kuingiza hatua mahususi zitakazochukuliwa, bajeti na malengo yanayopimika kwa kila sekta
  - Kama hufanyi kazi katika ngazi ya taifa, unaweza kuuliza mpango wa utekelezaji katika ngazi ya msingi (jimbo, kanda, mkoa, wilaya, nk)
  - (tafadhali angalia kwa pamoja vitu maalumu kwa mazingira yako, kwa mfano kama mpango wa utekelezaji haupo omba mpango mkakati wa kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake au kama mpango upo, omba ili uumarishe)

- Imarisha mipango mikakati ya taifa iliyopo kwa;
  - kufanya mipango inayo jumuisha sekta mbalimbali ,kuimarisha sekta ya afya, ustawi wa jamii, polisi, elimu, mahakama na jinsia
  - Ingiza mikakati ya ujengaji uwezo na uimarishaji wa mifumo ili kusaidia mkakati wa kuzuia na kushughulikia ukatili wenye mwitikio wa kijamii
  - kuwezesha mipango kupatikana hadharani na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyiwa tathmini ya mara kwa mara.
  - (tafadhali angalia kwa pamoja mambo gani maalumu ambayo ni mahitaji muhimu kwa mazingira yako, kwa mfano kama mpango upo, chambua na omba vitu hapo juu, ambavyo vinakosekana humo au kama hufanyi kazi katika ngazi ya taifa, rekebisha haya mahitaji kwa ngazi ya msingi kwa mfano mahitaji ya kuimarisha mipango ya kikanda / eneo / jimbo / wilaya)
- Anzisha mfumo wa utaratibu wa taifa wenye mamlaka ya kutosha na bajeti ya kuandaa, kutekeleza na kutathmini hatua ya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Kama unafanya kazi katika ngazi ya msingi, fikiria eneo / jimbo / mkoa / wilaya
- Kuhakikisha rasilimali zipo ili kusaidia utekelezaji wa kitaifa / mipango ya serikali za mitaa ndani ya wizara zote zinazohusika, na kwa ajili ya ushiriki wa harakati za wanawake / asasi za wanawake.

Kama umekamilisha karatasi kazi, Itakuwa rahisi kurekebisha mahitaji ya utetezi katika mazingira unayofanyia kazi.

## Sehemu D

- Sote tunaweza kuzungumza kwa uwazi na kutoa wito kwa viongozi wetu kuchukua hatua! Hebu tuwaulize waonyeshe uongozi na kuongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake sasa!


GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum›Fostering Activism